



GRETSA UNIVERSITY - THIKA

**UNIVERSITY EXAMINATIONS
MAY-AUGUST 2018 SEMESTER**

BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

KODI: KISW 102

KOZI: MBINU ZA MAWASILIANO KATIKA KISWAHILI

DATE: 8 AUGUST 2018

TIME: 3.00 PM – 6.00 PM

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. SEHEMU YA KWANZA **A**: NI YA **LAZIMA**
2. SEHEMU YA PILI **B**: JIBU MASWALI YOYOTE **MATATU**
3. **USIANDIKE CHOCHOTE** KWENYE KARATASI YA MTIHANI. KWA KUFANYA HIVYO UTAKUWA UMEVUNJA SHERIA ZA MITIHANI NA UTAADHIBIWA
4. ANDIKA VIDOKEZO VYAKO NYUMA YA **KIJITABU CHA MAJIBU** KISHA PIGIA MSTARI BAADAYE

TAHADHARI:- Kamera za CCTV zipo kwenye vyumba vyote vya mitihani

SEHEMU YA A: NI YA LAZIMA

Swali La Kwanza

- a) Mawasiliano ni nini? **[Alama 2]**
- b) Toa vijejezi vya dhana zifuatazo **[Alama 10]**
- i) Tanbihi
 - ii) Marejeleo
 - iii) Hotuba
 - iv) Uwakifishaji
 - v) Aya
- c) Ainisha vipengele vitano muhimu katika uwanja wa mawasiliano **[Alama 5]**
- d) Kwa msaada wa mchoro, fafania mchakato mzima wa mawasiliano. **[Alama 10]**
- e) Fafania kiutondoti mawanda manne ya mawasiliano katika suala zima la mawasiliano **[Alama 8]**
- f) Kozi hii ya Mbinu za Mawasiliano ina manufaa yepi kwako wewe kama mwanafunzi na vilevile mkufunzi mtayarishwa na mtarajiwa? **[Alama 5]**

SEHEMU YA B: JIBU MASWALI YOYOTE MATATU

Swali La Pili

- a) Pambanua hatua mwafaka za uandishi wa Insha katika mawasiliano. **[Alama 10]**
- b) Marejeleo katika kazi za kiakademia huwa na nafasi yake. Faragua kwa utondoti nafasi hii huku ukihimili majibu yako kwa mifano mwafaka. **[Alama 8]**
- c) Orodhesha aina 2 ya marejeleo unayofahamu. **[Alama 2]**

Swali La Tatu

- a) Ni vipi ishara zaweza kuwa kizingiti katika mchakato wa mawasiliano? [Alama 5]
- b) Umepewa nafasi ya kutoa maelekezo juu ya hotuba. Eleza jinsi utakavyoandaa hotuba tokea mwanzoni hadi jukwaani [Alama 15]

Swali La Nne

- a) Angazia sifa bainifu za mawasiliano ya:
- i) Mtandaoni [Alama 6]
 - ii) Magazetini
- b) Tofautisha kati ya mazungumzo ya Redioni nay ale ya Runinga. [Alama 4]
- c) Mukstadha ni muhimu sana katika mawasiliano. Changanua nafasi yake katika mazungumzo. [Alama 4]
- d) Pambanua aina za mawasiliano katika jamii na kutolea mifano faafu. [Alama 8]

Swali La Tano

- a) Tathmini kwa upana stadi ya uandishi kwa kujikita katika hatua muhimu za uandishi [Alama 10]
- b) Ni zipi tofauti za kimsingi zinazojitokeza kati ya stadi ya mazungumzo na ile ya maandishi? [Alama 10]

Swali La Sita

- a) Talii mikakati/dhamira 3 za uandishi wa insha. [Alama 9]
- b) Ni vipi mwandishi/msomi anaweza kukuza aya katika harakati ya kuandika isha yake [Alama 5]
- c) Ainisha mambo yanayozingatiwa katika kuhariri na kusahihisha insha yako. [Alama 3]

AHERI